



BODI YA KAHAWA TANZANIA

TANGAZO

UFUNGUZI WA MSIMU WA KAHAWA 2020/2021

Utangulizi

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Kahawa Tanzania anawatangazia ufunguzi wa msimu mpya wa ununuzi wa kahawa kwa mwaka 2020/2021. Tangazo hili linatolewa kwa mujibu wa kanuni ya 23 (1) ya Kanuni za Kahawa 2013. Pamoja na tangazo hili, Bodi inatoa mwongozo na utaratibu mahsusi kuhusu utaratibu wa masoko ya kahawa kwa mujibu wa kanuni ya 63 ya Kanuni za Kahawa 2013.

Tarehe za ufunguzi wa msimu wa kuanza kwa ununuzi wa kahawa katika kanda za uzalishaji kahawa ni kama ifuatavyo;

Na.	Kanda	Mkoa	Tarehe ya Ufunguzi
1.	Kaskazini	Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Morogoro, Tanga	1 Julai, 2020
2.	Mbeya, Songwe	Mbeya, Songwe, Katavi	1 Juni, 2020
3.	Kigoma	Kigoma	1 Mei, 2020
4.	Mara	Mara, Mwanza	1 Juni, 2020
5.	Kagera	Kagera	1 Juni, 2020
6.	Ruvuma	Ruvuma, Iringa, Njombe	1 Julai, 2020

Mambo muhimu ya kuzingatia katika msimu huu 2019/2020:

1. Wanunuzi binafsi na wenye viwanda wanaruhusiwa kununua kahawa kutoka kwa wakulima moja kwa moja kwa kupitia vyama vya Ushirika vya Msingi na vyama vikuu (Union). Kahawa itakayonunuliwa katika soko hili ni ile ambayo imepitia utayarishaji ngazi ya awali (*Dry Cherry na Parchment*). Wanunuzi wa kahawa watakaotaka kununua kahawa katika soko hili watatakiwa kuwa na leseni za kununua kahawa zinazotolewa na Bodi ya Kahawa kwa mujibu wa sheria ya kahawa na kanuni zake (Parchment Buyers Licence & Dry Cherry Buying Licence). Wanunuzi hawa watapaswa kuingia makubaliano na chama cha ushirika husika yatakayoonyesha kiasi na bei ya kahawa itakayotolewa na mnunuzi wa kahawa.

Wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya kwa kuzingatia kifungu Na. 26 (2) na Na. 38(5) cha kanuni ya kahawa ya mwaka 2013 watatoa vibali kwa wanunuzi wa kahawa kwenye Halmashauri zao ikiwa ni moja ya masharti ya kupata leseni ya ununuzi kutoka Bodi ya Kahawa.

2. Katika msimu huu Bodi ya Kahawa Tanzania itaendelea na utaratibu wa kuendesha minada katika kanda za uzalishaji kahawa katika maeneo yafuatayo:
 - **Bukoba:** Kwa ajili ya Mikoa ya Kagera, Mwanza – Minada itaendeshwa kama kutapatikana kiasi cha kahawa cha kutosha kuendesha minada.
 - **Mbozi:** Kwa ajili ya Mikoa ya Songwe, Mbeya, Iringa na Katavi
 - **Mbinga:** Kwa ajili ya Mikoa ya Ruvuma na Njombe

Minada ya kanda itaendelea kuwa ni ya kahawa safi na itafanyika kwa mujibu wa kanuni na taratibu za uendesaji minada zilizopo. Minada wa kitaifa unaofanyika Moshi utaendelea kufanyika kwa taratibu zilizopo na vyama vya ushirika vitakuwa huru kuchagua soko wanaloliona lina tija kwa kuuza kahawa ya wanachama wao.

3. Katika msimu huu utaratibu wa soko la moja kwa moja (Direct Export) kwa kahawa aina ya Robusta na Arabika ngumu utakuwa ni kama ulivyoboreshwa msimu uliopita ambapo Vyama vya Ushirika vitatangaza kiasi cha kahawa wanachotarajia kuzalisha kwa madaraja na ubora kupitia tovuti ya Bodi ya Kahawa, Soko la Bidhaa (TMX) na Tume ya Maendeleo ya Ushirika na muda ambao kahawa itakuwa tayari.

Wanunuzi wa kahawa kupitia mfumo wa soko la moja kwa moja watawasilisha mapendekezo yao ya bei kwa Bodi ya Kahawa yakiainisha yafuatayo;

- i. Kiasi na aina ya kahawa kwa kila daraja.
- ii. Ubora wa kahawa.
- iii. Muda/mwezi ambao wanatarajia kuchukua kahawa husika.
- iv. Bei anayotarajia kulipa kwa kila daraja la kahawa kwa kuzingatia utaratibu wa bei ya soko, muda wa ununuzi na ubora wa kahawa.

Mapendekezo ya bei yaliyowasilishwa na wanunuzi wa kahawa yatashindanishwa kupitia utaratibu utakaokuwa unasimamiwa na Bodi ya Kahawa na Soko la Bidhaa (TMX) na matokeo yatawasilishwa kwa Vyama vya Ushirika kwa makampuni yaliyotoa bei ya juu ili vyama hivyo viweze kuingia makubaliano ya kuuza kahawa kwa washindi hao kupitia utaratibu wa soko la moja kwa moja au kwa wanunuzi wengine watakaoweza kutoa bei kubwa zaidi ya mshindi. Bei halisi ya kahawa katika makubaliano hayo itafikiwa wakati wa kuchukua kahawa.

4. Maombi ya leseni zote mpya yatafanyika kwa kutumia mtandao katika mfumo wa ATMIS kwa kufuata kiungo cha <https://atmis.kilimo.go.tz>. Kwa wale watakaokuwa wanahuisha leseni zao watajaza fomu maalum ya kuomba kuhuisha leseni zao itakayopatikana kwenye tovuti ya Bodi ya Kahawa www.coffeeboard.or.tz

5. Vyama vya ushirika vinatakiwa kuanza kukusanya kahawa kutoka kwa wakulima mara tu inapokuwa tayari. Aidha, vyama vya ushirika vitapaswa kuhakikisha kuwa akaunti zao za malipo zipo hai ili kuwezesha zoezi la uuzaji wa kahawa na malipo kufanyika mapema na kuepuka ucheleweshwaji wa malipo ya fedha za wakulima.
6. Vyama vya msingi vilivyopewa kibali cha kuuza kahawa mnadani msimu uliopita vitahuisha vibali vyao kwa kujaza fomu maalum. Fomu hizi zitapatikana kwenye ofisi za Kanda za Bodi ya Kahawa na kwenye viwanda vya kukobolea kahawa.
7. Vyama vya ushirika vikamilishe mapema taratibu za upatikanaji wa mitaji ili vianze ukusanyaji wa kahawa ya wakulima wao mara tu kahawa inapokuwa tayari.
8. Bodi ya Kahawa itaanza mara moja kuendesha minada ya kahawa pindi kiasi cha kutosha cha kahawa kitakapokuwa tayari.
9. Vyama vya ushirika vihakikishe kuwa mitambo ya kuchakata kahawa (CPU) iliyoko chini yao inatumika na inafunguliwa mara tu kahawa inapokuwa tayari ili kufanikisha lengo la Serikali la kuongeza ubora wa kahawa na bei ya mkulima.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu
Bodi ya Kahawa Tanzania
S. L. P. 732 – Moshi
Simu: 027-27-52324
Nukushi: 027-27-52026
Barua pepe: info@coffeeboard.or.tz
Tovuti: www.coffeeboard.or.tz



DECLARATION OF THE 2020/2021 COFFEE BUYING SEASON

Preface

The Director General of the Tanzania Coffee Board (the Board) hereby declares to the general public the commencement of the 2020/2021 coffee buying season as per Regulation No. 23 (1) of the Coffee regulation, 2013. Additionally, the Board hereby issues specific guidelines in relation to marketing procedures of coffee during the 2020/2021 coffee buying season as mandated by Regulation No. 63 of the Coffee Industry Regulations, 2013.

The 2020/2021 coffee buying season shall commence on the following dates and in the following coffee growing zones;

No.	Zone	Region	Commencement Date
7.	Northern Zone	Kilimanjaro, Arusha, Manyara, Morogoro, Tanga	1 st July, 2020
8.	Southern Highlands Zone	Mbeya, Songwe, Katavi	1 st June, 2020
9.	Kigoma Zone	Kigoma	1 st May, 2020
10.	Mara Zone	Mara, Mwanza	1 st June, 2020
11.	Western Zone	Kagera	1 st June, 2020
12.	Southern Zone	Ruvuma, Iringa, Njombe	1 st July, 2020

Important factors for consideration during the 2020/2021 coffee buying season:

10. Private buyers who own coffee processing factories will be permitted to buy parchment coffee (Dry Cherry and Parchment) directly from farmers through their respective Primary Societies and Cooperative Unions after obtaining the relevant licence from the Board according to existing laws, regulations, rules and guidelines (Parchment Buyers Licence & Dry Cherry Buying Licence). Buyers interested to buy coffee at this market will be required to enter into agreements with the relevant primary society (Amcos) or Union stipulating the quantity and price of coffee being offered by the coffee buyer.

District Executive Directors will issue permits to these buyers in accordance with Regulations 26 (2) and 38 (5) of the Coffee Industry Regulations, 2013 being one of the conditions to be fulfilled before licences are issued by the Board.

11. During the 2020/2021 coffee buying season, the Board will continue conducting auctions at the zonal level in all coffee growing zones as shown hereunder;
 - **Bukoba:** To cater for Kagera and Mwanza Regions – These auctions will only be conducted if there will be adequate amounts of coffee to conduct Auction.
 - **Mbozi:** To cater for Songwe, Mbeya, Iringa and Katavi Regions.
 - **Mbinga:** To cater for Ruvuma and Njombe Regions.

Zonal coffee auctions will sell clean coffee (green beans) only, and shall be conducted in accordance with the existing auction procedures. The national coffee auction will also be conducted in Moshi and Cooperatives are at liberty to choose which market through which their coffee will be sold after weighing the advantages gained to their members.

12. The procedure for Direct Export sale of Robusta and Hard Arabica coffee shall remain the same as it was during the previous coffee season (2019/2020) whereby Cooperatives will publish on TCB, TMX's and Cooperative Development Commission's (TCDC) websites information on the amount of coffee they anticipate to produce, when their coffee will be ready to enter the market including details of grades and the quantity of coffee which will be offered for sale.

Prospective buyers of coffee through the Direct Export market will be required to submit their offers to the Board stipulating the following details;

- v. The quantity, grade and each type coffee.
- vi. The quality of the coffee.
- vii. The time frame within which the coffee should be delivered to the buyer.
- viii. The anticipated price to be paid per grade of coffee according the procedures, market prices, delivery month and the quality of the coffee.

The submitted offers will be subjected to competition which will be conducted jointly by Tanzania Coffee Board (TCB), (TMX) and TCDC. Thereafter the highest bidders will be submitted to the respective Cooperative for considerations to facilitate completion of Direct Sale agreements. Should the highest bidder fail to purchase the coffee, the unions will be at liberty to sell their coffee to the next available bidder with the highest price. The final price of purchase will be ascertained upon delivery of the coffee to the buyer.

13. All fresh licence applications for the new coffee buying season will be submitted electronically via the ATMIS system through the following link <https://atmis.kilimo.go.tz>. All applicants who are renewing their licences will be

required to fill a specific form requesting renewal of their licence; the said form will be available on TCB website www.coffeeboard.or.tz

14. All Cooperatives and Unions are required to commence coffee collection from their respective members promptly upon its availability and to process the same without delay at Coffee Milling factories. Furthermore, Cooperative Unions are required to ensure that all the relevant bank accounts are active to enable expedient sale and payment of farmers' coffee proceeds without delay.
15. All primary societies seeking renewal of their auction permits will be required to apply for renewal by filling the requisite forms which will be available at all the Board's zonal offices and coffee milling factories.
16. All Cooperative Unions are required to complete all financial preparations early on to facilitate timely collection of coffee upon its availability.
17. The Board will commence sale of coffee via auction promptly upon availability of adequate stocks of coffee.
18. Cooperatives are urged to ensure that all Central Processing Units (CPU) within their respective areas are operating and utilized expediently and as soon as coffee is available for processing in order to support the Government's objective of increasing the quality and the price of coffee for the farmers' benefit.

Acting Director General
Tanzania Coffee Board
P.O. Box 732 – Moshi
Telephone: 027-27-52324
Facsimile: 027-27-52026
Email: info@coffeeboard.or.tz
Website: www.coffeeboard.or.tz